# THE FINAL CURVE

## K.C.P.E TRIAL -2020

# -KISWAHILI-

## SEHEMU YA KWANZA: LUGHA

**Muda: Saa 1 Dakika 40**

**SOMAKWAMAKINIMAAGIZOYAFUATAYO**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibu. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lionyeshe katika **KARATASI YAM A JJBU** na wala sio katika kijitabu cha maswali.

**JINSIYAKUTUMIAKARATASIYAMAJIBU**

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu

**NAMBARI YAKO YA MTIHANI**

**JINALAKO**

**JINALASHULEYAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye nambari zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani nambari ya shule. Na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alamazozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu
9. Kwa kila swali 1-50 uniepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambayo ni sahihi. Chagua jibu hilo
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilojibu.

**Mfano:**

**Katika kijitabu cha maswali:**

19. Kamilishi methali: Ukiona vyaelea jua______
A. vyaenda
B. vimeundwa
C. vyazima
D. vyaisha

[D] |

Jibu **sahihi** ni B.

EE er ED i1 a cl i r Era ie EE a eo

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba **19,** kisanduku chenye herufi **B** ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

== am

Ecolebooks.com

-

**Kitabu hiki cha maswali kina kurasa 8 zilizopigwa chapa.**

C) ***umetungwa na kuchapishwa na Tangent Ventures***

FUNGUA UKURASA

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

*Soma vifungu vifuatavyo. 1 na nafasi Impaka 1. Kwa kila nafasi unepewa majibumanne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya vale uliyopewa.*

Sarufi ya Kiswahili ___I___vipengee vingi sana ambavyo havina budi___2___barabara na kwa undani na watu wote___3___lugha hii ya Kiswahili. ____l azima yeyote anayejifunza Kiswahili ajue nomino ambata ___"__O___. Isitoshe, ajue maana za methali kama mwanamke mzuri hakosi kilema humaanisha 7

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A.inazo | B. inao | C. inacho | D.inavyo |
| **2.** | A. kufaharniwa | B. kufahamisha | C. kufahamikwa | D. kufahamishwa |
| **3.** | A. wangejifunza | B.watajifunzao | C. wajifunzao | D. waliojifunzao |
| **4.** | A.Lakini | B.Aidha | C. Badala | D. Bali |
| **5.** | A. mithili | B. labda | C. bila | D. mathalani |

6. A.kimya, shughuli, dalili B.mjamzito, kipimamvua, mjusikafiri
   C.chuma, saa, kifuhiko D. Kabarak, Arusha, Malindi

7. A. heri kuwa na kitu kibaya kuliko kukosa
   B. hapana binadamu asiyekuwa na upungufu au udhaifu fulani
   C. mtoto huwa kama mzazi wake
   D. kila mtu anaweza kupata ulemavu

Saidi alizaliwa na ___8___ katika familia ___9___. Wazazi wake walikuwa wafanyabiashara__10____waliosafiri nchini na ng'ambo kwa shughuli hizo. Hata hivyo, Saidi alikuwa kijana___11___. Alikuwa na mazoea ya kuwatukana watu na hata kuwapiga watoto wengine___12___Jambo___13__1iliwahuzunisha sana wazazi wake. Baba yake___14___ushauri kuwa heshima si____15____lakini aliyatia masikio yake pamba.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **8.** | A.kulezwa | B. kulelewa | C.kulewa | D.kuleka |
| 9. | A. isiyojiweza | B.iliyojiwezesha | C. isiyojiwezesha | D.iliyojiweza |
| **10.** | A.maalum | B.maamuma | C.maarufu | D.maafu |
| **11.** | A.mtundu | B.rnpole | C.rnkubwa | D.mnene |
| **12.** | A.: | B .. | C. () | D.; |
| **13.** | A. hilo | B.hiyo | C.hayo | D.hizo |
| **14.** | A. alirnpea | B.alimpa | C.alimwuliza | D. alimrudishia |

Ecolebooks.com

**15.** A.utume B.ujumbe C.utumwa D.unafikii



DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

***Kutoka swali la 16_30, iibu swali kulingana na maagizo uliyopewa,***

**16.** Chagua orodha iliyo na vokali pekee

A. ch, dh, th, sh

B. b, p. th, dh

C. e, o, u, i

D. a, b, k, n

17. *"Tutaenda kucheza baada ya masomo."* **Wanafunzi walisema.** Katika usemi taarifa ni:

A. Wanafunzi walisema tutaenda kucheza baada ya masomo.

B. Wanafunzi walisema wataenda kucheza baada ya masomo.

C. Wanafunzi walisema kuwa wangeenda kucheza baada ya masomio.

D. Wanafunzi waliomba kwenda kucheza baada ya masomo.

**18.** Ni sentensi ipi iliyotumia kiunganishi sahihi?

A. Naomba unipe wala shilingi kumi ninunulie andazi.

B. Usile minghairi ya kunawa.

C. Aghalabu hukupita mtihani, hutapata tuzo leo.

D. Watoto watiifu hadi hupendwa na walimu.

**19.** Chagaa sentensi yenye 'kwa' ya sababu

A. Tuliandamana bega kwa bega hadi uwanjani.

B. Amepandishwa cheo kwa uaminifu wake.

C. Kuimba kwa Bahati hufurahisha watu wengi.

D. Katika insha nilipata alama thelathini kwa arubaini.

**20.** Baraza nila wazee na __ __ ni la nyuki.

A. bunda

B. shumbi

C. kaumu

D. bumba

**21.** Chagua kinyume cha;

***Kapera ameingia ndani ya nyumba ya shaibu.***

A. Mwanamwali ametoka nje ya nyumba ya ajuza.

B. Mseja ametoka nje ya nyumba ya buda.

C. Mwanamwali ametoka ndani ya nyumba ya Mzee.

D. Mseja ameingia ndani ya nyumba ya

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

kijana.

22. Chaguajibu lenye maelezo sahihi

A. Nauli ni malipo ya kuingia kwenye ukumbi au sinema.

B. Kiangazamacho ni malipo ya kumshikia moto kwa mara ya kwanza.

C. Kiinuamgongo ni malipo ya mtu aliyestaafu.

D. Fidia ni malipo ya adhabu inayotozwa kortini.

23. Vifaa hivi vya ufundi vinajulikana kama

| i | ii |
|---|---|
| A. bisibisi | shepe |
| B. shepe | sururu |
| C. atepe | filifili |
| D. sururu | patasi |

24. Kanusha sentensi hii:

***Ungevaa nguo ungehisijot0.***

A. Usingevaa nguo usingehisi joto

B. Hungevaanguo hungehisijoto.

C. Ungevaa nguo usingehisi joto.

D. Ungevaa nguo hungehisi joto

25. Ikiwa mtondo itakuwa Jumatano, leo ni:

A. Jumamosi

B. Ijumaa

C. Jumapili

D. Jumatatu

26. Malizia methali hii

***Palipofia ndege hapakosi*** ______

A. manyoya

B. mayai

C. makinda

D. mifupa

27. Bainisha aina ya maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi hii

Mtoto wao amesimama wimamlangoni.

A. Kivumishi kimilikishi, kitenzi, kielezi

B. Kivumishi, kielezi, kihusishi

C. Kivumishi, kielezi, kielezi

D. Kivumishi kimilikishi , kielezi, kiunganishi

28. Chagua sentesi yenye matumizi sahihi ya kiulizi.

A. Je? Unaweza kukaa siku ngapi bila chakula.

B. Salale? Hujui tofauti kati ya mbu na mbung'o!

C. Haambiliki hasemezeki? Hawezi kushauriwa.

D. Nilimshinda mpinzani mkubwa sembuse wewe usiyekuwa na chochote?

29. Tegua kitendawili hiki:

***Ziwa la kwetu twaogelea kandokando.***

A. Uji

C. Moto B.

Joto

D. Kidimbwi

30. Sentensi hii itakuwaje katika hali ya ukubwa?


***Mkia wa mbuzi ulikatwa kwa kisu***

A. Kia la buzi lilikatwakwajisu.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

B. Mamkia ya mbuzi yalikatwa kwa visu. C. Jikia lajimbuzi lilikatwa kwa iikisu .. D. Kikia cha kibuzi kilikatwa kwa kijisu.





***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 mpaka 40.***

Ingawa viungo vyote vya mwili ni muhimu, nafikiri kuwa jicho ni sehemu muhimu zaidi. Jicho ni kiungo cha mwili kinachotumiwa kuonea au kutazamia. Ukiwauliza vipofu watakuambia kwa kinywa kipana kuwa ni afadhali kuumia mkono au mguu kuliko kuumia jicho. Macho yakipoteza uwezo wake wa kuona, ulimwengu wa mtu hujaa giza na aghalabu mtu hushindwa kujifanyia mambo bila udhia.

Hii ina maana kuwa lazima na sharti kila mmoja ayatunze macho yake. Hatuna budi kuyatunza na kulinda macho dhidi ya maambukizi. Afya nzuri ya macho hutegemea kwa kiasi kikubwa virutubishi vinavyopatikana katika vyakula tulavyo. Virutubisho kama Omega 3, Zinki na Vitarnini C na E husaidia kupunguza hatari ya magonjwa ya macho.

Mtoto wa jicho ni kitu chenye rangi nyeupe ambacho huota kwenye jicho na kumfanya mtu ashindwe kuona vizuri. Tatizo hili linaweza kupunguzwa kwa kula vyakula vyenye virutubisho. Retina ni sehemu ya jicho ambayo hupokea nuru ndani ya jicho. Retina hupokea taarifa ambayo ni mwanga wa kitu unachokiona kisha kuisafirisha taarifa hiyo kwenda kwenye ubongo iii ubongo uweze kufanya utambuzi wa kitu hicho ni nini hasa. Retina inapochoka mtu hushindwa kutambua vitu anavyoviona. Kuchoka kwa retina kunaweza kusuluhishwa kwa ulaji wa vyakula vyenye virutubisho.

Kupata virutubisho vyote hakikisha sahani yako haikosi vyakula kama: mboga za kijani kama spinachi, mchicha na sukumawiki. Aidha, zoea kula samaki, mayai (zingatia mayai ya Kienyeji), machungwa na matunda mengine yenye uchachu. Kumbuka kuwa lishe salama ambayo ina wanga na sukari kidogo pamoja na vyakula vya mafuta kama nazi, parachichi na samaki, kwa wingi itakusaidia kukuepusha na kuugua maradhi ya kisukari. Kisukari ni chanzo mojawapo cha upofu.

Utafiti umeonyesha kuwa uvutaji sigara husababisha kuchoka haraka kwa retina na kushindwa kufanya kazi. Hili husababisha wingu kwenye mboni ya jicho. Kama hujaanza kuvuta sigara usianze hata kidogo. Kwa wale ambao kila wakijaribu kuacha kuvuta sigara wanashindwa, hawana budi kutafuta msaada wa madaktari.

Njia nyingine ya kutunza macho ni kupunguza matumizi ya vifaa vya kielektroniki vinayotoa mwangaza mkali kama kompyuta, simu na televisheni. Mwangaza mkali unaotolewa na vifaa hivi husababisha uchovu wa macho. Pia hufanya macho kutoona vizuri na kuwa na mawenge. Vilevile huleta maumivu ya shingo, mabega na mgongo. Kulinda macho yako hakikisha kuwa unatumia miwani maalum ya kuzuia athari ya miale ya mwangaza wa vifaa vya kielektoniki.

Iwapo unafanya kazi zinazohitaji matumizi makubwa ya kompyuta, hakikisha kuwa kila baada ya dakika ishirini hivi unapumzisha macho kwa kuangalia pembeni au juu kwa sekunde thelathini.

Ecolebooks.com

Hali kadhalika epuka michezo mibaya kama ya kucheza kwa vijiti usije kujeruhiwa machoni. Yote tisa, kumi ni kwamba ni muhimu kwa kila mmoja wetu kwenda hospitalini kufanya vipimo na uchunguzi wa macho mara kwa mara. Hasa kwa watoto, itasaidia kugundua magonjwa mapema na kuyatibu. Kinga ni bora kuliko tiba.



DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

**31.** Kulingana na aya ya kwanza;

A. Jicho si sehemu muhimu kama viungo vingine.
B. Viungo vyote vina umuhimu ingawa jicho ni muhimu zaidi.
C. Watu wasioweza kuona hutumia midomo badala ya macho.
D. Kuumia mkono au mguu ni kuzuri zaidi.

**32.** Kifungu kimebainisha kuwa macho yakipoteza uwezo wake wa kuona;

A. Dunia nzima huwa na giza.
B. Mtu hushindwa kujifanyia mambo.
C. Mtu hupata shida katika shughuli zake.
D. Hutamani kuumia kiungo kingine.

**33.** Chagua jibu ambalo si sahihi kulingana na aya ya pili:

A. Mtu ana hiari ya kutunza macho yake.
B. Afya nzuri ya macho hutegemea vyakula tulavyo.
C. Omega 3, Zinki na Vitamini hupunguza hatari ya magonjwa ya macho.
D. Ulaji wa vyakula vyenye virutubisho hupunguza hatari ya maambukizi ya magonjwa ya macho.

**34.** Chagua jibu sahihi kulingana na kifungu.

A. Virutubisho vinavyopatikana katika vyakula humaliza kabisa magonjwa ya macho.
B. Athari ya mtoto wa jicho hufanya mtu asiwe na uwezo wa kuona kabisa.
C. Afya ya macho hutegemea virutubisho vipatikanavyo katika vyakula pekee.
D. Ingawa kuna njia nyingine za kutunza macho, ulaji wa vyakula vyenye virutubisho ndiyo njia kuu.

**35.** Kwa mujibu wa aya ya tatu:

A. Mtu anapochoka retina hushindwa kutambua vitu anavyoviona
B. Ulaji wa vyakula kunaweza kusuluhisha tatizo la kuchoka kwa retina
C. Retina huhusika kwa kiwango kikubwa kufanikisha utambuzi wa ubongo kwa kile kilichoonekana.
D. Retina ni sehemu ya jicho ambayo hutuma nuru ndani ya jicho.

Ecolebooks.com

**36.** Ni kipi si kirutubishi cha kusaidia kupunguza ugonjwa wa macho?

A. Omega3

B. Zinki

C. Vitamini C

D. Vitamini D

37. Mwandishi anapinga hali gani hasa katika aya yasita?

A. Upatikanaji wa wingu kwenye mboni ya jicho.

B. Uvutaji wa sigara.

C. Kutafuta msaada wa madaktari.

D. Retina kushindwa kufanya kazi.

**38.** Ipi hapa haijatajwa kama njia ya kutunza macho?

A. Kukoma kabisa kutumia vifaa vya kielektroniki.

B. Kuepuka uvutaji wa sigara.

C. Ulaji wa vyakula vinavyofaa.

D. Kuepuka michezo hatari inayoweza kujeruhi.

**39.** Neno **'pembeni' lina maana gani kama** lilivyotumiwa?

A. Mbali

B. Mbele

C. Katikati

D. Kando

**40.** Uchunguzi wa macho ni muhimu kwa vile:

A. Husaidia kuepuka mambo yanayodhuru macho.

B. Husaidia kugundua magonjwa mapema na kuyadhibiti.

C. Husaidia waliotumia kompyutakwanjia isiyofaa.

D. Hukinga macho ya mtu kutokana na magonjwa



DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

***Soma Kifunga kifuatacho kishaujibu maswali 41-50.***

Ilitokea wakati ambapo ukosefu wa nafasi za kazi ulikita mizizi. Uikuwa vigumu sana kupata kazi yoyote ile. Hata wale waliokuwa na elimuya kiwango chajuu pia walij ipata wakiathiriwana hali hii. Wakati huo msemo wa: ***Kazi ni kazi bora mkono uende kinywani'*** ulipata umaarufu mkubwa. hawakuchagua wala kubagua kazi. "Bora kazi si kazi bora', ndivyo walivyosikika wakisemavijana wengi waliokuwa wakitafuta kazi.

Ilitokea kuwa Zuzu bin Juha alikuwa mmoja wa ***waliokula mwande*** katika utafutaji wa kazi. Kutwa kucha Zuzu bin Juha alizunguka katika pembe zote za mtaa wao akitafuta kazi yoyote. Alinuia kupata kazi ajikimu yeye mwenyewe. Licha ya hayo, kishawishi kikubwa cha kusaka ajira kilikuwa kumsaidia mama yake aliyekuwa ni mlemavu. Kwa ndege mzuri, Zuzu bin Juha aliajiriwa kazi na tajiri mmoja aliyeitwa Lalaheri. Kazi yenyewe ilikuwa si ngumu kama zile za wafanyakazi wengine kwenye boma la Lalaheri. Kazi yake ilikuwa rahisi kama nini! Ilikuwa kazi ya kunadhifisha bustani la Bwana Lalaheri peke yake.

Ingawa wakati mwingine angehitajika kufunga na kufungua lango kuu, hiyo siyo iliyokuwa kazi yake kuu. Alifanya hivyo tu endapo bawabuhakuwapo au alikuwa ameenda likizoni. Katikati ya boma la Lalaheri palikuwa na mti mkubwa sana wa injakaranda. Mti huo mkubwa ulipendeza na kurembesha mandhari kwa maua yenye rangi ya urujuani na yenye sura ya tarumbeta na majani madogo madogo.

Mti huo licha ya uzuri wake ulipukutisha na kuangusha majani kila wakati. Mintaarafu ya hayo, kazi kubwa ya Zuzu bin Juha ilikuwa ni kuyafagia majani yaliyopukutishwa na mti huo. Kazi hiyo aliifanya vizuri sana. Daima hakukosajifagio kubwa mkononi.

Kazi hiyo ilimpendeza sana mwajiri wake. Hata kabla ya muda waliokuwa wameagana kuwa angemwongeza mshahara kufika, Lalaheri alimwongezea mshahara maradufu. Kuongezewa mshahara huku kulimpa motisha Zuzu binJuha wa kufanya boma liwe safi zaidi.

Wakati mwingine Zuzu alipokuwa hafagii, hafyeki wala kupura na kupogoa nyua, angewapa mkono wafanyakazi wengine. Mathalani angewasaidia wajakazi katika kazi zao kama kuchanja kuni, kukun~ nazi, kupara samaki miongoni mwa kazi nyingine nyingi. Hili lilifanya mwajiri ampende na kumchukulia kama mtoto wake mwenyewe.

Nyakati za wikendi, Lalaheri alipokuwa akipeleka familia kwa madhari au pikiniki alimwomba Zuzu bin Juha kuandamana nao. Maisha yake Zuzu yalibadilika yakawa ya kutamaniwa na wengi. Hata nyama zilimkubali! Alinenepa na kuwa tambo la mtu. Alikuwa mtanashati, wangeandamana na Lalaheri, ungedhani Zuzu ndiye naye Lalaheri ni mwajiriwa. Siku moja Zuzu alimwendea mwajiri na kumwambia, "Aisee! Nimepata suluhu latatizo la majani yaangukayo na kuchafua mazingira!" Lalaheri alimpa ruhusa ya kufanya alivyoona ikiwa vyema. Zuzu hakupoteza wakati, alitwaa shoka na kuuangusha mjakaranda huo. Aliukatakata vipande vipande na kuuchanjachanja kuwa kuni. Alipofagia pahali hapo baada ya kuking'oa kisiki cha mti wenyewe.

Furaha aliyokuwa nayo Zuzu ilikuwa haina mfano. Alijua kuwa kazi yake ingekuwa rahisi sana. Jioni hiyo Lalaheri alipofika alishangaajinsi boma lilivyokuwa safi. Zuzu alimwelezea kwa furaha lam vile alivyofanya. Lalaheri alimpongeza na kumwambia, "Mkono ulishao haukatwi!" Zuzu

Ecolebooks.com

hakuelewa maana ya maneno hayo. Alijua maana tu baada ya kupokea barua ya kupigwa kalamu. Machozi yalimtoka milizamu milizamu. Alikuwa amejimwagia unga wake mwenyewe. Mwiba wa kujidunga...



DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

41. Aya ya kwanza imedhihirisha kuwa:
A. Waliokuwa na elimu ya kiwango chajuu hawakuathirika kama wale waliokuwaa wamesoma.
B. Si kazi zote ambazo zilikuwa hazipatikani kwa urahisi.
C. Hali ya mambo ilifanya watu kuridhia kazi yoyote ile iliyopatikana.
D. Vijana ndio waliokuwa waathiriwa wakubwa wa tatizo la ukosefu wa kazi.

42. ***Kazi ni kazi bora mkono uende kinywani*** inaonyesha kuwa:
A. Matunda ya kazi hayawezi kuonekana kwa siku moja.
B. Kazi ya lazima huchosha na kumsumbua mtu kuliko kazi ambayo amejitolea kufanya.
C. Watu wanastahili kutegemea kazi zao badala ya kutegemea watu wengine.
D. Hakuna kazi iliyo bora mradi iweze kukidhi mahitaji ya anayeifanya.

43. Chagua jibu sahihi kwa mujibu wa aya ya tatu:
A. Licha ya kunadhifisha boma la Bwana Lalaheri, Zuzu aliajiriwa kufanya kazi ya langoni.
B. Kazi ya kufungua na kufunga lango ilikuwa ikifanywa kwa zamu kati ya Zuzu na bawabu.
C. Ingawa kazi ku ya Zuzu ilikuwa kusafisha boma, upo wakati aliposaidia kazi nyingine ilipobidi.
D. Mti mkubwa wa mjakaranda ulikuwaa karibu na lango la boma la Bwana Lalaheri.

44. ***'Mti huo, licha ya uzri wake, ulikuwa ukipukutisha na kuangusha majani kila wakati'***
Ni methali gani inayoweza kujumlisha ujumbe huu?

45. Kulingana na kifungu:
A. Zuzu alikuwa hajui jinsi ya kutunza mazingira.
B. Zuzu hakufahamu uhusiano wa kazi yake na mjakaranda.
C. Zuzu hakung'amua sababu ya mti kuwa kwenye boma.
D. Zuzu hakujua kufanya kazi aliyopewa.

46. Chagua tabia ya Zuzu kulingana na kifungu hiki
A. Mwenye bidii, mjinga.
B. Mwenye maarifa, mkwele.
C. Mwenye heshima, mvumilivu.
D. Mwenye busara, mkarimu.

47. Kauli, ***'Hata nyama zilimkubali'*** inamaanisha nini kulingana na hadithi hii?
A. Alikufa
B. Alikula nyama
C. Alinona
D. Alinenepa

48. Kifungu kimebainisha kuwa:
A. Zuzu alikuwa akitafuta kazi ya kujisaidia

A. Hakuna masika yasiyokuwa mbu.
B. Ila haifichiki, hujifichua yenyewe.
C. Ivumayo haidumu.
D. Kupata si kukosa.

***Tangent Ventures***

Ecolebooks.com

yeye mwenyewe.
B. Kitendo cha Zuzu kuukata mjakaranda kinadhihirisha kuwa alikuwa naujuzi wa kazi.
C. Lalaheri aliona hakuna haja ya kumwajiri Zuzu tena ilhali kazi yake ilikuwako.
D. Zuzu alikuwa na nia ya kuboresha utendakazi wake kwa kuukata mjakaranda.

**49.** Kauli, *'Mkono ulishao haukatwi'* ina maana kuwa:
A. Hapana haja ya kushindana na watu waliotuzidi nguvu.
B. Tuwasaidiapo watu na wao watatusaidia pia.
C. Tufanyapo jambo fulani tufikirie jinsi litakavyotuathiri
D. Hatufai kujeruhi kiungo cha mwili tutumiacho kulia chakula

**50.** *"Mwiba wakujidunga..."* Nukta tatu zilizotumiwa katika sentensi hii zinaitwa
A. Mabano
B. Dukuduku
C. Vistari
D. Nukta pacha



DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM